



JARIDA LA MTANDAONI
TOLEO NAMBA 173 | JULAI 02, 2022

SUMAJKT NI MAHALI SAHIHI KIBIASHARA NA UWEKEZAJI



Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Dkt. Stargomena Lawrence Tax (katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Mkuu wa JKT Meja Jenerali Rajabu Mabele (watatu kushoto) Mwenyekiti wa bodi ya SUMAJKT Meja Jenerali Farah Mohammed (watatu kulia) Mkuu wa Tawi la Utawala JKT Brigedia Jenerali Hassan Mabena (wapili kulia) Mkurugenzi Mtendaji wa SUMAJKT Kanali Petro Ngata (wapili kushoto) Mkuu wa Tawi la mahusiano JKT Kanali Aloyce Chagula (wakwaza kulia) Mkuu wa Tawi la sheria JKT Kanali Rutahiwa pamoja na wajumbe wa bodi ya SUMAJKT nje ya banda la JKT viwanja vya sabasaba jijini Dar es Salaam.

SUMAJKT NI MAHALI SAHIHI KIBIASHARA NA UWEKEZAJI

Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Dkt. Stergomena Lawrence Tax, amesema SUMAJKT ni mahali sahihi kibiashara na uwekezaji kwa kuwa kuna viwanda vinavyotengeneza bidhaa muhimu.

Mhe. Dkt. Stergomena Tax, amezungumza hayo tarehe 01 Julai 2022, alipokuwa akifunga maadhisho ya miaka 41 ya SUMAJKT kwenye uwanja wa maonesho ya kimataifa ya biashara sabasaba.

Aidha, Mhe. Dkt. Stargomena, ametoa wito kwa SUMAJKT kuangalia eneo kubwa ili kuhakikisha shirika linajitanua na kuwekeza sahemu mbalimbali hasa katika miradi ya kitaifa.

"SUMAJKT ipo tayari kushirikiana na mtu yoyote atakayehitaji ujuzi anakaribishwa." Amesema Mhe. Dkt. Stargomena Tax.

Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Dkt. Stargomena Lawrence Tax, amefafanua kuwa kwa sasa kuna masoko ya kibiashara ya nje ili kufikia masoko hayo lazima uzalishe bidhaa zinazokidhi ubora wa kimataifa.

Ili kuweza kupita katika masoko ya kibiashara ya nje lazima bidhaa zikidhi mambo matatu ambayo ni ubora, kiwango kinachotakiwa na kufikisha hicho kiwango kinachohitajiwa kwa wakati.

Ameongeza kuwa masoko ya nje yaliyopo ni Kanda huru ya Afrika Mashariki na Kanda ya Jumuiya ya Kusini mwa Afrika.

Nae Mkuu wa JKT na Afisa Mtendaji Mkuu wa SUMAJKT Meja Jenerali Rajabu Mabele, amesema kuwa Shirika hilo limekuwa likitoa gawio kwa Serikali kila mwaka na mwaka huu wa fedha SUMAJKT limetoa zaidi ya shilingi bilioni moja.

Aidha, Meja Jenerali Mabele, ameongeza kuwa Maendeleo ni makubwa tangu SUMAJKT lilipoanza mpaka sasa hivi, pia SUMAJKT limesaidia kwa kiwango kikubwa kupunguza tatizo la ajira nchini.

Kwa upande wa Mkurugenzi Mtendaji wa SUMAJKT Kanali Petro Ngata, ameeleza kuwa Shirika linashiriki maonesho ya 46 kimataifa ya biashara sabasaba ambayo yanaenda sambamba na maadhisho ya miaka 41 ya SUMAJKT tangu kuanzishwa kwake mwaka 1981.

Ameongeza kuwa maonesho hayo yaliyofunguliwa rasmi tarehe 29 Juni yatahitimishwa tarehe 13 Julai 2022.

Pia amesisitiza umuhimu wa Watanzania kujitokeza kuhesabiwa ifikapo 23/8/2022 kwa maendeleo ya taifa na Watanzania kwa ujumla.

Matukio Katika Picha

**Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe.
Dkt. Stargomena Lawrence Tax, akisaini
kitabu cha wageni katika banda la JKT
alipowasili viwanja vya sabasaba jijini
Dar es Salaam.**



**Mkuu wa JKT na Afisa Mtendaji
Mkuu wa SUMAJKT Meja
Jenerali Rajabu Mabele, akisaini
kitabu cha wageni alipowasili
katika viwanja vya maonesho
ya 46 kimataifa ya biashara
sabasaba jijini Dar es Salaam.**

**Mkuu wa JKT na Afisa Mtendaji
Mkuu wa SUMAJKT Meja
Jenerali Rajabu Mabele
(kushoto) akijadili jambo na
Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri
SUMAJKT (wapili kushoto)
pamoja na Mkurugenzi
Mtendaji SUMAJKT Kanali
Petro Ngata (wakwanza kulia)
katika viwanja vya maonesho
ya 46 kimataifa ya biashara
sabasaba jijini Dar es Salaam.**



Matukio Katika Picha

Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Dkt. Stergomena Tax (aliyevaa barakoa) akimsikiliza Mkuu wa JKT Meja Jenerali Rajabu Mabele (aliyeinua mkono) alipotembelea banda la JKT kwenye maonesho ya 46 ya kimataifa ya biashara sabasaba jijini Dar es Salaam.



Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Dkt. Stergomena Tax (aliyevaa barakoa) akimsikiliza Meneja mradi wa ufugaji samaki (SUMAPONICS) Meja Kelvin Ngondo(aliyevaa fulana nyekundu) alipotembelea banda la JKT kwenye maonesho ya 46 ya kimataifa ya biashara sabasaba jijini Dar es Salaam.



Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Dkt. Stergomena Tax (aliyevaa barakoa) akimsikiliza Meneja Kiwanda cha samani Chang'ombe Meja Hemed Mchwanga (aliyevaa fulana nyekundu) alipotembelea banda la JKT kwenye maonesho ya 46 ya kimataifa ya biashara sabasaba jijini Dar es Salaam.